Mfanya Biashara Mwenye Mafanikio Aliyeshindwa

na

Ellis P. Forsman

Mfanya Biashara Mwenye Mafanikio Aliyeshindwa

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 8, 2011

Mfanya Biashara Mwenye Mafanikio Aliyeshindwa

Luka 12: 16-21

Luka 12:16-21, *"Akawaambia methali akisema, shamba la mtu mmoja tajiri lilikuwa limezaa sana. Akanza kuwaza moyononi mwake, akisema nifanyeje? Maana sina pakuyaweka akiba mavuno yangu. Akasema, nitafanya hivi, nitazivunja ghala zangu nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu. Kasha nitajiambia, Ee nafsi yangu una vitu vyema vingi ulivyojiwekea hakiba kwa miaka mingi pumzika basi, ule, unywe, ufurahi. Lakini Mungu akamwambia mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka Roho yako, na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba asijitajirishe kwa Mungu."*

Kama kunakitu katika ulimwengu huu ambayo tungeweza kuchukia kuwa, ni kwamba tushindwe. Lakini tajiri mpumbavu ambaye tumesoma habari zake katika kifungu hicho ni kwamba alishindwa kiukweli.

Alikuwa mwenye mafanikio makubwa, alikuwa ni mfanya biashara mwenye mafanikio. Hakuwa mkulima mdogo, bali alimiliki na kuendesha mashamba makubwa.

Kama ningekuwa mwana sanaa, ningechora picha ya huyu mtu aliefanikiwa na kuliweka katika shamba kubwa huko Texas. Karibia juu ya picha, pembeni kidogo, ningeweka miinuko inayozunguka iliyofunikwa na kijani kibichi ambapo ng'ombe waitwao Texas White-faced Hereford zilikuwa zina chungiapo. Chini ya picha ningeweka uwanja wa mimea. Baada ya hapo ningeweka mji mzuri. Karibu na hapo ningeonyesha ghala kubwa. Popote katika picha, ningemweka mkulima huyu akiwa amekaa katika farasi mkubwa akiangalia eneo lake.

Kuipa jina picha hii, ningeweka katika maneno haya: "mtu mwenye mafanikio." Lakini Mungu akachukua cha kupakia rangi mkononi mwangu badala yake nikaandika maneno haya "mtu aliyeanguka vibaya."

Katika macho ya ulimwengu, mtu huyu alikuwa katika utukufu wa mafanikio, lakini katika macho ya Mungu alikuwa mtu aliyeanguka vibaya sana. Ulimwengu unapomtaza na kukiri kwamba ni tajiri, Mungu alimuita mpumbavu. Ulimwengu ungemuita mbabe hakuna mwingine, lakinia Mungu anamuita mjinga.

Kwa nini alikuwa mjinga? Habu na tuangalie ni kwa nini.

Alimuacha Mungu Nje ya Maisha yake

Zaburi 9:17, *"Wadhalimu watarejea kuzimu, naam, mataifa yote wanaomsahau Mungu"*

Katika mipangilio yake yote, hakika alimuacha Mungu nje. Aliongelea *"matunda yangu", "maghala yangu" "vitu vyangu".*

Mungu alimpa huyu mtu vyote alivyoitaji ili kuwa na mafanikio: mwili wenye nguvu na afya, kupambazuka, na mvua, mzunguko wa mhula, aridhi yenye rutuba, hivi vyote vili wezesha mafanikio yake.

Alitupa baadhi ya mbegu katika aridhi na katika kila fundo limoja la mkononi Mungu alimwongezea. Mungu alimpatia kila kitu nay eye hakupenda kumpa Mungu kitu kama zawadi.

Tabia ya Napoleon.

Napoleon alipanga kuingilia Urusi na kumshinda Kaesaria. Mtu mmoja akasema katika uwepo wake, "mwanadamu anapendekeza, lakini Mungu hapendekezi." Ali muacha Mungu kwa njia ya ovyo, na ikadhihirishwa kosa. Kwa sababu Mungu alimshughulikia kupitia mmoja wa wadogo zake na wingi wa vimbe- viakukimbilia kwenye barafu. Majeshi yake hayakujiandaa kwa ajili ya barafu ya Urusi, na alishindwa. "Urusi itakuwa yangu," moyo wake wenye kiburi ulisema, lakini Mungu alikuwa pale.

Mtu anayekwenda katika biashara na kumsahau Mungu anatengeneza anguko kubwa. Kama anashindwa kumchukua Mungu wa mbingu kama mwenza na msuluhishi, ameelekea kushindwa, kwa sababu katika kitabu cha Mungu ina patikana njia salama ya kanuni zote na mbinu za uchumi na viwanda.

Aliwaacha binadamu wenzake nje ya maisha yake

Huyu mtu mpumbavu aliyemsahau Mungu pia aliwasahau majirani zake.

Hakumwambia mke wake, "tuna nafaka nyingi, mahindi, matunda, na mboga mboga ambavyo hatutazitumia. Tuna paswa kuwapelekea majirani zetu ambao hawana chakula.

Kirahisi alisema, *"Nitafanyia nini mali zangu?"*

Yesu akafundisha kwamba "*Amri kuu nay a kwanza"* ni:

Math. 22:37-39, *"Yesu akamwambia,mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa nafsi yako yote, na kwa akili yako yote. Hii*

ndio amri kuu nay a kwanza. Na ya pili inafanana na hii, mpende jirani yako kama nafsi yako."

Lakini mtu huyu mjinga alivunja amri hizi zote.

Adith ya kweli ya upendano wa ndugu:

Mama Chiang Kai-shek alitoa simulizi ya shujaa wa uchina mashamba ya mpunga wakati wa tetemeko la aridhi. Akiwa katika uwa wa juu ya shamba lake alihisi tetemeko la aridhi na kuona kwa mbali bahari ina mawimbi yakitoka katika mfumo wao wa zamani. Alijua kwa bahari itarudi katika hali yake ya kawaida. Katika korongo chini, alimwona jirani yake akifanya kazi katika shamba ambalo lingeangamizwa na maji. Alijua kwamba usalama wao ungekuwa katika mwinuko juu ambapo alikuwepo, na kwamba walipaswa kufika pale haraka. Hakungekuwa na maana kuwaita, labda wasingesikia kwa umbali huo. Haraka akakimbilia maghala ya mpunga ambayo yalikauka. Akiwa na tochi aliwasha moto ghalani kwake. Majirani zake wakaona moshi na wakakimbia kwenda katika mwinuko na kumsaidia. Alafu kutokana na kuwepo kwao salama katika mwinuko waliangalia mwelekeo wa bahari aliponyosha. Waliona maji yakifunika sehemu ambayo wali kimbia kutoka. Kidogo, walijua wokovu wao na kile kilicho garimu Yule aliyewaita. Tukio waliloweka akilini mwake bado lina simama, akiwa na kauli mbiu, "Alitupatia vyote alivyo kuwa navyo, na alitoa kwa furaha.

Mtu mjinga ambaye Yesu aliongela alifikiri nafsi ya mwanadamu inaweza kuridhishwa na vitu vya kimwili.

Luka 12:19, *"Kisha nitajiambia, Ee nafsi yangu, unavitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi."*

Kunakitu kuhusu nafsi ya mwana damu ambayo haiwezi kuridhishwa na vitu vya kimwili na vina aribika.

Math.4:4, *"Akajibu na kusema, imeandikwa, mwanadamu hataishi kwa mkate peke yake, bali kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mungu."*

Furaha kuu iliyoko katika ulimwengu huu mra zote haipo katika wale ambao wana furaha katika shaba na fedha na maisha mazuri kila siku. Watu wengi wanaishi katika unyenyekevu na amani, wakati wengine wanaishi katika raha na mali huwa wana shida katika kulala kwao.

Pesa haiwezi kuleta furaha iliyo kamili na kutimiza matakwa yetu yote.

- Mhubiri 5:10, "*Apendaye fedha hatashiba fedha, wala apendaye wingi hatashiba nyongeza. Hayo pia ni ubatili."*

- Mhubiri 4:6, *"Heri konzi moja pamoja na utulivu, kuliko konzi mbili pamoja na taabu, na kujilisha upepo."*

Alifikiri kwamba alikuwa na pumziko zuri katika maisha

Luka 12:19, *"Kisha nitajiambia ,Ee nafsi yangu, unavitu vyema vingi ulivyojiwekea hakiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi."*

Hatujui kinachotusubiria kesho.

- Mithali 27:1, *"Usijisifu kwa ajili ya kesho, kwa maana hujui yatakayozaliwa na siku moja."*
- Yakobo 4:14, *"Walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka."*

Hakuna mtu mwenye afya katuka dunia hii anayetarajia kuwa katika kaburi lake kati ya miaka 6 ijayo. Labda hutarajii kuwa katika kaburi lako kwa miaka 6 ijayo.

Vile vile, inawezekana kuwa jeneza limesha tengenezwa ambalo mwili wa mmoja wetu labda utalazwapo. Kwa hiyo, Mungu akamwambia mtu huyu, *"wewe mpumbavu."* Hivyo, hakuwa tayari kuonekana wa ovyo; hakutaka mtu yeyote amuongoze katika jamii. Bado Mungu alimwona mjinga.

Hatimaye Mungu akamwambia, "*usiku huu nafsi yako itahitajika kwako."* Mtu huyu aliongelea kuhusu kesho; lakini Mungu aliongelea SASA. Alafu Mungu akamwambia, *"baadaye vitu hivyo vitakuwa vya nani, ambazo wewe hutajagawia watu?"*

Nyumba ambayo wewe unaishi siku moja itakaliwa na wengine, ikitunza muda wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Hakiba na vitu ulivyotunza na pesa zako katika benki, ambayo sasa unadai kuwa ni vyako, vita milikiwa na wengine, baada yaw ewe kuonda katika dunia hii, kwa sababu zitabaki nyuma.

1 Tim. 6:6-10, *"Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kuondoka na kitu; ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tama nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. Maana shina moja ya mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani wamefarakana na imani, na kujichoma kwa maumivu mengi."*

Hatimaye, Mungu anatuambia:

Luka 12:21, "*Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaya nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu."*

"Ndivyo alivyo" – Yeye nani? Mtu yeyote – wewe, mimi, hao wote walioweka imani yao katika vitu vya dunia na "siyo matajiri kwa Mungu."

- Math. 6:19-20*, "Msijiwekee nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba. Bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusipoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi."*

- 1 Tim. 6:17-19, "*Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kwa kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; uku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima uliyo kweli kweli."*

Hitimisho

Mhubiri 12: 13-14, *"Hii ndiyo jumla ya maneno yote yamekwisha sikiwa; mche Mungu, nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo ipasavyo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya."*

Kama unafanya kosa kama ambalo mtu huyu alifanya:

- Ukifikiri kwamba una pumziko katika maisha.

- Ukifikiri kwamba kuna muda mwingi wa kumkubali Kristo; muda mwingi wa kujiandaa na umilele.

Nakutaka ujinufaishe na uzuni ambayo mtu huyu alipitia.